

## **KIUMBE KIPYA** **Na Ndugu Robert Stapleton**

Kama Wakristo ni muhimu kutambua sisi ni nani. Sio tu tunavyopaswa kuwa. Na wala tutakavyokuwa. Bali kama Wakristo sisi ni nani. 2 Wakorintho 5:17, 18 inabainisha kwamba kila Mkristo ni “kiumble kipy”.

Endapo tutaelewa hili tutaanza kuishi katika namna ambayo Mungu anatutazamia kama viumbe vipy. Wakristo wengi wa mdomoni bado wanaishi kwa namna ile ile walivyokuwa wanaishi kabla ya kuwa Wakristo. Na wote wanatakiwa wategemee kushangaa Siku ya hukumu (Mathayo 7:21-23). Katika makala hii, hebu tuone baadhi ya mambo yahusikayo kuwa kiumble kipy.

### **KIUMBE KIPYA KINA UHUSIANO MPYA NA MUNGU**

Upya huu ni kutokana na badiliko la uhusiano kwenye sheria ya Mungu (Yohana 3:18). Hapo awali pale mtu anapofanyika kuwa Mkristo, asiyé Mkristo hushindwa kuendana na sheria ya Mungu katika maeneo mengi. Dhana inayosemwa na baadhi ya watu, kwamba mwanadamu hawezu kuwa chini ya sheria ya Mungu kabla hajaitii injili ni kejeli. Dhambi ni uasi juu ya sheria ya Mungu (1 John 3:4). Aliye ndani ya Kristo ameachiliwa (amesamehewa) hizi dhambi zote na kwa hiyo, hakabiliwi na hukumu inayotokana na alivyovunja sheria ya Mungu kabla hajawa ndani ya Kristo (Warumi 8:1). Na kwa nyongeza, Mungu anakuwa Baba yao, pamoja na haki zote za kuweza kuwaambia watoto wake anayotaka watende na yale asiyootaka wasitende (1 Yohana 3:1, 2; Mathayo 7:21). Yeye, Baba ana haki ya kuwarudi hao watoto Waerania 12:7).

### **KIKUMBE KIPYA KINA UHUSIANO MPYA NA UTAWALA WA MUNGU**

Ingawa Waefeso 2:12 inalenga kuzungumzia Mataifa (wasio Wayahudi), lakini fungu hili la maandiko hutupa ujumbe muhimu kuhusu uhusiano wetu na utawala wa Mungu. Kimsingi, twaona ya kuwa Biblia inaonyesha kwamba kiumble kipy ni mwenyeji na ni watakatifu, na mrithi sawa sawa na ahadi za Mungu (Waefeso 2:19; Warumi 8:17). Mgeni anapopewa uraia, anakuwa mtu mpya kiuhusiano na serikali yetu. Kanuni hiyo hiyo huhusika kwa kiumble kipy katika Kristo kwa kuzingatia ufalme wa Mungu wa kiroho.

### **KIUMBE KIPYA KINA UHUSIANO MPYA NA MWENZAKE**

Anayefanyika Mkristo anakuwa na uhusiano mpya na kanisa na ulimwengu kwa pamoja. Kwa upande wa kanisa, sasa anakuwa sehemu yake (Matendo 2:47). Kwa upande wa ulimwengu, sasa anajitahidi kutoupenda tena (1 Yohana 2:15-17). Mtu huyu anapokuwa kiumble kipy hali yake ya kale inakuwa imebadilika kabisa—“Ya kale yamepita”. Anakuwa kiumble kutokana na majukumu yake, kwa kuwa sasa anamatumikia Bwana (Mathayo 6:24). Kiumble kipy hukabiliwa na fursa mpya ambazo hazikujitokeza hapo kabla (Wagalatia 6:10)

### **KIPYA KIPYA HUWA NA MAPITO MAPYA**

Kuwa kiumble kipy haimaanishi kuwa siku zote ataishi kwenye kilele cha mlima. Na wala hajaelezwa kuwa hatutapata magumu na hatutasikitishwa (kukatishwa tamaa). Ni

kwa sababu tu uhalisia mpya unaogusa na kuboresha kila pito lake unakuwa umeingia katika maisha yake (Warumi 8:28). Mtu anapofanyika kuwa kiumbe kipyta, ufahamu wa uwepo wa ulinzi huja ambaa haukupata kuwapo kabla (Mathayo 28:20). Mtu napofanyika kuwa kiumbe kipyta, anakuwa mnufaika wa baraka mpya za rohoni ambazo hazikuwa zinapatikana kwake ( Waefeso 1:3). Ujasiri unapatikana kwa kujua kuwa yuko upande sahihi, hata ingawa anaishi katika ulimwengu uliojaa dhambi (Wakolosai 1:20). Tumaini linakuwa ndilo chembe ya thamani katika pito hili jipya (Tito 1:2)

### **KIUMBE KIPYA NI KIUMBE KIPYA KATIKA KITOVOU CHA NAFSI YAKE**

Tunapoongelea kufanyika kiumbe kipyta ni lazima tuelewe kwamba tunaongelea hali itokayo katika utu wa ndani ( Ezekieli 36:26). Kiumbe hiki kipyta kinakuwa kimezaliwa upya (Yohana 3:3). Sio tukio la kubadilika tu kutoka katika hali ya kale kwenda hali mpya, bali ni kufanyika upya kwa ile iliyokuwa ya kale (Warumi 6:4). “Utu wa kale” unakuwa umefishwa na tunakuwa tumefufuliwa ili tuenende katika upya wa uzima (Warumi 6:4, 6). Tumewekwa huru mbali na dhambi (Warumi 6:18). Tumeanza upya kama vile ambavyo tungenza upya endapo tungezaliwa upya kimwili.

Je,wewe u kiumbe kipyta? Sijauliza kama umebatizwa?. Nimeuliza, wewe u kiumbe kipyta?